

# Kaunti ya Orleans Sasa Inastahili Msaada wa FEMA

---

**Release Date: Julai 27, 2023**

Ufadhili wa serikali sasa unapatikana ili kuwasaidia watu binafsi katika kaunti ya ziada ya Vermont kurejelea hali kawaida baada ya dhoruba kali, mafuriko, maporomoko ya ardhi na maporomoko ya matope kuanzia Julai 7, 2023 na kuendelea.

Wakaazi wa Kaunti ya Orleans ambao nyumba zao au mali zao za kibinafsi ziliharibiwa wanaweza kutuma maombi ya msaada wa majanga kwa FEMA. Kaunti za ziada zinaweza kuongezwa baadaye ikiwa serikali itaomba na kuthibitishwa na matokeo ya tathmini zaidi za uharibifu.

Kaunti ya Orleans ni pamoja na kaunti nane ambazo tayari zimeteuliwa kwa Msaada wa Mtu Binafsi: Caledonia, Chittenden, Lamoille, Orange, Rutland, Washington, Windham na Windsor.

Msaada unaweza kujumuisha ruzuku kwa ajili ya ukarabati wa nyumba na makao ya muda, mikopo ya riba nafuu ili kufidia mali iliyopotea isiyo na bima na programu nyinginezo za kuwasaidia watu binafsi na wamiliki wa biashara kurejelea hali ya kawaida baada ya majanga.

Ili kutuma ombi la msaada, piga simu kwa Laini ya msaada ya FEMA kwa 800-621-3362 kati ya saa moja asubuhi (7 a.m.) na saa tano usiku (11 p.m.); nenda mtandaoni kwa [DisasterAssistance.gov](https://www.disasterassistance.gov); au pakua [FEMA App](#). Ikiwa unatumia huduma ya usambazaji kama vile huduma ya usambazaji video (VRS), huduma ya simu iliyo na maelezo mafupi au nyinginezo, pea FEMA nambari yako ya huduma hiyo unapotuma ombi.

Kwa habari za hivi punde tembelea [fema.gov/disaster/4720](https://www.fema.gov/disaster/4720). Fuata akaunti ya FEMA Region 1 katika Twitter [twitter.com/FEMARegion1](https://twitter.com/FEMARegion1) au ukurasa wa Facebook katika [facebook.com/FEMA](https://www.facebook.com/FEMA).



**FEMA**

Page 1 of 2

Kwa masasisho kuhusu itikio na msaada wa Vermont, fuata Wakala wa Usimamizi wa Dharura wa Vermont [twitter.com/vemvt](https://twitter.com/vemvt) kwenye Twitter na Facebook [facebook.com/vermontemergencymanagement](https://facebook.com/vermontemergencymanagement).

FEMA imejitolea kuhakikisha msaada wa majanga unatekelezwa kwa usawa, bila ubaguzi kwa misingi ya rangi, dini, utaifa, jinsia, umri, ulemavu, ujuzi wa Kiingereza au hali ya kiuchumi. Mwathiriwa yeyote wa majanga au mwananchi anaweza kuwasiliana na Ofisi ya Haki za Kiraia ya FEMA ikiwa anahisi kuwa amethiriwa na ubaguzi. Ofisi ya Haki za Kiraia ya FEMA inaweza kupatikana bila malipo kwa 833-285-7448. Maopareta wanaotumia lugha mbali mbali wanapatikana.



**FEMA**

Page 2 of 2